HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MPANGO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI MISITU

KIJIJI CHA NANJIRINJI A

MISITU YA MBUMBILAA&B

MPANGO HUU UMEANDALIWA NA SERIKALI YA KIJIJI CHA CHA NANJIRINJI A

MARCH 2018 MPAKA FEBRUARY 2023

YALIYOMO

1: UTANGULIZI 3
1.1 Umiliki wa Msitu 3
1.2 Lengo Kuu la Mpango wa Usimamizi 3
1.3 Madhumuni 3
1.4 Mfumo wa Usimamizi 3
1.5 Muda wa Utekelezaji na Marekebisho ya Mpango 4
2: HISTORIA FUPI YA MPANGO 5
2.1 Jamii 5
2.1.1 Hali ya Kiuchumi na Kijamii 5
2.2 Maelezo kuhusu Misitu 5
2.2.2 Hali ya Udongo 6
2.2.3 Uoto wa Asili na Mazingira. 6
2.2.4 Jamii za Miti ya Mbao 6
2.2.5 Mazao Yasiyotimbao 7
2.2.6 Wanyama Pori na Jamii za Ndege 7
2.3 Maeneo ya Usimamizi. 7
2.3.1 Msitu wa Mbumbila A 7
2.3.2 Msitu wa Mbumbila B 8
2.4.1 Mambo ya Asili & Haki za Kijadi 8
2.4.2 Historia ya Nyuma 8
2.4.3 Matumizi ya Sasa 8
3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU. 9
3.1 Matumizi ya Msingi 9
3.2 Matumizi Huru ya Misitu 9
3.3 Shughuli katika Misitu Zitakazotozwa Ushuru 9
3.4 Mazao Yanayohitaji Vibali vya Uvunaji 9
3.4.1 Utaratibu wa Kupata Leseni ya Uvunaji Miti ya Mbao. 11
3.5 Matumizi Yasiyoruhusiwa ndani ya Msitu 12
4: HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU 14
4.1 Kijiji 14
4.1.1 Haki 14
4.1.2 Manufaa 14
4.1.3 Majukumu ya Serikali ya Kijiji 14
4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili 15
4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji 16
4.2 Halmashauri ya Wilaya 16
4.2.1 Haki 16
4.2.2 Manufaa 16
4.2.3 Majukumu 17
4.3 Serikali Kuu 17
4.3.1 Majukumu 17

4.4 Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's) 17

4.41 Majukumu *17*

5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU **18**

5.1 Mikakati ya Jumla ya Kuendeleza Msitu 18

5.2 Ulinzi wa Misitu 18

5.2.1 Ushirikishwaji wa Jamii katika Ulinzi wa Misitu *18*

5.2.2 Walinzi wa Doria *19*

5.3 Kusafisha Mipaka na Barabara za Moto 19

5.4 Kurudisha hali ya Misitu 19

5.4.1 Kutokana na Machipukizi (Uoto wa asili) *19*

5.4.2 Upandaji wa miti kwenye maeneo yaliyo wazi *19*

5.4.3 Palizi kwenye maeneo yaliyopandwa miti *20*

6: MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU **21**

6.1 Vyanzo vya Mapato 21

6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau 21

6.3 Matumizi ya Mapato 21

6.4 Ukusanyaji na Utunzaji wa Fedha 22

6.4.1 Vitabu Muhimu vya Kutunza Kumbukumbu Vinavyotakiwa *22*

6.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi *22*

6.4.3 Kuwajibishwa *22*

7: UFUATILIAJI NA TATHIMINI **24**

7.1 Ufuatiliaji 24

7.2 Tathimini ya Kati na ya Mwisho 24

KIAMBATISHO A : RAMANI INAYOONYESHA MIPAKA YA KIJIJI **26**

KIAMBATISHO B : RAMANI INAYOONYESHA MIPAKA YA MISITU YA KIJIJI **27**

i. Ramani inayoonyesha Mipaka ya Misitu wa Kijiji –Mbumbila A. *27*

ii. Ramani inayoonyesha Mipaka ya Misitu wa Kijiji –Mbumbila B *28*

KIAMBATISHO C : MPANGO WA UTEKELEZAJI **29**

KIAMBATISHO D : VIWANGO VYA USHURU **31**

KIAMBATISHO D: SHERIA NDOGO **32**

SURA YA KWANZA

1: UTANGULIZI

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 inatoa kipaumbele kwa jamii kushirikishwa katika usimamizi wa misitu. Pia Sera inasisitiza mchango wa sekta ya misitu katika kukuza kipato cha jamii ili kupunguza umasikini. Mwaka 2002 Serikali ya Tanzania ilipitisha sheria mpya ya misitu ambayo inaipa mamlaka jamii zinazoishi kandokando ya misitu kusimamia misitu yao. Kijiji cha Nanjirinji A kimeandaa mpango wa matumizi endelevu wa Msitu wa Kijiji. Matumizi haya yameainishwa katika mpango huu wa Usimamizi Misitu.

Mpango huu ni mwongozo wa shughuli zote zitakazofanyika katika kipindi cha miaka mitano cha kutumika kwa mpango na shughuli hizo zimefafanuliwa na kuwekwa bayana. Shughuli hizo ni uboreshaji wa msitu, usimamizi, udhibiti wa uvunaji haramu, usimamizi wa sheria za misitu na ukusanyaji na usimamizi wa mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali za msitu. Kutakuwa na utunzaji wa kumbukumbu za shughuli zote zilizofanyika ili kuendana na matakwa ya mpango. Kumbukumbu zote zitapatikana pia katika Halmashauri ya Wilaya. Sheria ndogo zimetungwa ili kusimamia utekelezaji wa mpango.

Mpango huu umeandaliwa na Kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Nanjirinii A, timu ya wawezeshaji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwa kushirikiana na Shirika la Kuhifadhi Mpingo(MCDI). Mpango huu utatumika katika kipindi cha miaka mitano.

1.1 Umiliki wa Msitu

Misitu inamilikiwa na Serikali ya Kijiji cha Nanjirinji A. Msitu wa kwanza (Mbumbila A) wa Kijiji cha Nanjirinji A wenye hekta 57641ulitengwa kuwa hifadhi mwaka 2012 na wa pili (Mbumbila B) wenye hekta 18,987ulitengwa 2016, misitu yote ilitengwa chini ya usaidizi wa kitalaamu toka kwa wawezeshaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwa kushirikiana na Shirika la kuhifadhi Mpingo na Maendeleo (MCDI).

1.2 Lengo Kuu la Mpango wa Usimamizi

Misitu ya Mbumbila A na Bilitengwa kwa lengo la kulinda, kuhifadhi, na kufanya uvunaji endelevu wa mazao ya misitu, mazao timbao na rasilimali zingine za misitu. Lengo kuu likiwa ni kuweka misitu katika hali ya uasilia na kuboresha hali ya maisha ya kizazi kilichopo na kijacho kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za Misitu.

1.3 Madhumuni

Kuboresha hali ya maisha ya wanajamii wa kijiji cha Nanjirinji A kwa;

1 Kuhifadhi maeneo yenye ukubwa wa hekta 57641na 18,987ya Misitu ya Kijiji chaNanjirinji A dhidi ya ukataji miti ovyo, uharibifu na matumizi yasiyofaa.

2 Kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji wa mazao yasiyo timbao kwa wakati wote kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

3 Kijiji cha Nanjirinji A kupata mapato kutokana na biashara ya rasilimali za misitu ili kuboresha maisha ya wanakijiji wake.

1.4 Mfumo wa Usimamizi

Usimamizi misitu ya asili unaofuata uvunaji endelevu, upandaji wa miti ya asili, utunzaji wa machipukizi na udhibiti wa moto kwa kufuata mpango uliopo.

1.5 Muda wa Utekelezaji na Marekebisho ya Mpango

i. Huu ni mpango wa miaka mitano. Mpango huu utarekebishwa na Kamati ya Maliasili mwishoni mwa mwaka wa pili au muda wowote endapo kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Hakutafanyika mabadiliko yeyote katika mpango huu bila ya kibali cha Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

ii. Baada ya kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji, mpango huu utafanyiwa mapitio ili kuwa na Mpangomwingine wa miaka Mitano.

iii. Mapendekezo ya Maboresho yataandaliwa na kujadiliwa na kamati ya Maliasili, na kuwasilishwa kwenye Halmashauri ya kijiji, na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

iv. Kamati ya maliasili na Halmashauri ya kijiji wanapaswa kushauriana na Afisa Misitu Wilaya, na/au wadau wengine wa maswala ya misitu, kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu wa kijiji kwa ajili ya kupitishwa na Mkutano Mkuu.

v. Afisa Mtendji wa kijiji akishirikiana na kamati ya maliasili, ataandaa taarifa za mabadiliko ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu, na kuziaambatanisha na muhtasari wa Mkutano mkuu wa kijiji uliothibitisha mabadiliko hayo, na kuziwasilisha kwa Afisa misitu wa Wilaya.

SURA YA PILI

2: HISTORIA FUPI YA MPANGO

2.1 Jamii

Kijiji cha Nanjirinji A kipo katika kata ya Nanjirinji, Tarafa ya Nanjirinji katika Wilaya ya Kilwa. Kutokana na Sensa ya Mwaka 2012, Kijiji kina idadi ya watu wapatao 5,130 katika kaya zipatazo 762, na kina hekta zipatazo 175,7323. Kilisajiliwa mwaka 1974 kabla kilikuwa kitongoji cha Nanjirinji.

Kijiji cha Nanjiriji A kinapakana na Kijiji cha Nanjirinji B kilichopo Kata ya Nanjirinji kwa upande wa mashariki, kwa upande wa magharibi kinapakana na Kijiji cha Milui kilichopo Wilaya ya Liwale,kwa upande wa Kaskazini kinapakana na Kijiji cha Likawage kilichopo Kata ya Likawage na Kusini kinapakana na Wilaya ya Ruangwa.

Kijiji hakina Cheti cha Ardhi cha Kijiji lakini mipaka inajulikana vizuri na Kijiji kina mihutasari ya makubaliano kuhusu mipaka pamoja na vijiji vyote vinavyopakana na Nanjirinji A. Mipaka ya kijiji imewekwa mawe ya kuonyesha alama za mipaka. Angalia Kiambatisho A. Ramani ya inayoonyesha ardhi ya Kijiji katika Wilaya ya Kilwa.

Vitongoji vya Kijiji vinavyotambulika ni: Naungo, Ndandawala na Nanjirinji A, kati ya hivyo Kitongoji cha Ndandawala kipo karibu na Misitu ya Kijiji.

2.1.1 Hali ya Kiuchumi na Kijamii

Wanajamii walio wengi ni wakulima. Wengine hujishughulisha na ufugaji na biashara ndogo ndogo.

Mazao makuu yanayozalishwa Kijijini kwa ajili ya chakula ni Mpunga, Mahindi, Mtama, Mihogo, Kunde, Ndizi na Miwa.

Mazao makuu yanayozalishwa Kijijini kwa ajili ya biashara ni Ufuta, Korosho na Karanga.

Mapato yatokanayo na kilimo kwa kila kaya ni kati ya Tsh500,000/= na Tsh 3,000,000/= kwa mwaka.

Wakulima hujipatia pato la ziada kutokana na uvunaji mbao, uwindaji na ufugaji nyuki.

Kila kaya ina wastani wa watu 7.

Huduma za jamii zinazopatikana Kijijini ni: Shule, Msikiti, Kituo cha afya, mawasiliano ya simu na Visima vya maji (4).

Wananchi huteka maji toka kwenye visima ambapo kwa miguu ni mwendo wa dakika5-10 toka katikati ya Kijiji.Vyanzo vya maji vingine katika vitongoji ni Mto Nakiu na Mto Mawerenje.

Mji ulio jirani na Kijiji ni Ruangwa ambao unafikika kwa pikipiki mwendo wa masaa 2 na gari mwendo wa saa moja.

2.2 Maelezo kuhusu Misitu

Majina ya misitu ni **Mbumbila A na Mbumbila B**.

2.2.1Mahali Misitu ilipo na Ukubwa Wake

Misitu ya Kijiji cha Nanjirinji A ni Mbumbila A na Mbumbila B ambapo msitu wa Mbumbila A una ukubwa wa hekta **57,641**naupo upande wa magharibi katika ardhi ya Kijiji. Unapakana na eneo la akiba upande wa kaskazini, Kitongoji cha Ndandawala na

Msitu wa Taifa wa Malei upande wa Mashariki, Wilaya ya Ruangwa upande wa kusini na Kijiji cha Milui kilichopo Wilaya ya Liwale. Msitu wa Mbumbila B wenye ukubwa wa hekta **18,987**upo upande wa Kaskazini mwa ardhi ya Kijiji. Unapakana na Kijiji cha Likawage kwa upande wa kaskazini, Msitu wa kijiji cha Nanjirinji B kwa upande wa Mashariki,Msitu wa Mbumbila A kwa upande wa kusini na Msitu wa wazi kwa upande wa magharibi. Angalia Kiambatisho B (i na ii), michoro inaoonyesha alama za mipaka ya misitu ya kijiji.

Misitu hufikika kwa kupitia barabara za Likawage na safari Club

Matumizi ya maeneo yanayozunguka misitu hii ni kama ifuatavyo;

- Kwa msitu wa Mbumbila A,upande wa kusini hakuna matumizi yoyote ya kijamii bali msitu umepakana na mto Mbwemkulu na Wilaya ya Ruangwa,upande wa kaskazini pia hakuna matumizi yoyote ya kijamii bali msitu umepakana na msitu wa hifadhi wa Taifa uitwao Malei,upande wa Magharibi pia hakuna matumizi yoyote ya kijamii bali msitu umepakana na Wilaya ya Liwale na upande wa Mashariki matumizi ni kilimo katika kitongoji cha Kitochi.
- Kwa msitu wa Mbumbila B,upande wa kusini hakuna matumizi yoyote ya kijamii bali msitu wa kijiji umepakana na msitu wa hifadhi wa Taifa wa Malei,upande wa kaskazini pia hakuna matumizi yoyote ya kijamii bali msitu umepakana na kijiji cha Likawage,upande wa Magharibi hakuna matumizi yoyote ya kijamii bali msitu umepakana na kijiji cha Mirui na upande wa Mashariki pia hakuna matumizi yoyote ya kijamii bali msitu umepakana na msitu wa hifadhi ya kijiji cha Nanjirinji B.

2.2.2 Hali ya Udongo

Aina ya udongo katika misitu hii ni mfinyanzi, udongo mweusi, tifutifu na kichanga.

Hali ya kijiografia ya misitu ni milima, tambarare na mabonde kiasi

2.2.3 Uoto wa Asili na Mazingira.

Sehemu kubwa ya misitu hii ni tambarare.

Uoto wa asili ni wa miombo (misitu ya mataji wazi). Miti mifupi ya miombo ndio inayopatikana kwa wingi zaidi na kuna vichaka vya miiba na uwanda wa nyasi hapa na pale. Pia kuna misitu mizuri ya ukanda wa mito na uwanda wa misitu ya pwani.

2.2.4 Jamii za Miti ya Mbao

Kuna aina nyingi za jamii tofauti za miti katika misitu ya Kijiji.

Kwa msitu wa Mbumbila A jamii ya miti ya thamani ya mbao iliyopo msituni ni Mkongo (*Afzelia quanzesis),* Mninga jangwa *(Pterocarpus angolensis),* Mpangapanga (*Millettia Stuhlmanii),* Mpingo (*Dalbergia melanoxylon),* Msenjele *(Acacia nigrescens)* , Msufi pori *(Bombax rhodognaphalon),* Mnidu *(Cordyala africana),* Mchenga *(Brachystegia speciformis),*Mlondondo *(Xeoderis stuhlmanii),* Mkunya,Mnepa,Mtanga, MtumbitumbiMlipa deni, Mpupi, Mgongo naMkwaju

Kwa msitu wa Mbumbila B jamii ya miti ya thamani ya mbao iliyopo msituni ni Mkongo (*Afzelia quanzesis),* Mninga jangwa *(Pterocarpus angolensis),* Mpangapanga (*Millettia Stuhlmanii),* Mpingo (*Dalbergia melanoxylon),* Msenjele *(Acacia nigrescens),* Mwembeti *(Sterculia quinquiloba),* Msufi pori *(Bombax rhodognaphalon),*Mnidu

(Cordyala africana), Mtondoro (Julbenardia globiflora), Mchenga *(Brachystegia speciformis),* Mlondondo *(Xeoderis stuhlmanii),Mgelegele,Mgongo* na Mkunya.

2.2.5 Mazao Yasiyotimbao

Kuna aina mbalimbali za mazao yasiyo timbao katika misitu hiiKama vile asali ya nyuki, uyoga, matunda pori, wanyama Pori, madawa ya asili na kamba. Miti inayofaa kwa ujenzi katika misitu yote miwili ni Mtalawanda, Mpweke, Mtapuche, Mnepa, Mtachi, Kingonogo, Kimbiha, Mkorobonjo, Galabachi, Mpunju, Mngambakamba na Mkiu.

Miti ya matunda kwa misitu hii ni Mtopetope, Mmbingi, Mfulu, Mangombe, Manjichi, Mtogo na Mbuyu na mingineyo.

Miti inayotumika kutengenezea kamba katika misitu hii ni Mtumbu, Mkamba, Mkiu, Mnepa, Myombo, Mmbalembale,Mchenga, Myombo na Msekese.

Jamii za uyoga zinazopatikana katika misitu hii ni pamoja na Mbuyu, Mkwaya, Kichuguu, Kitovu, Mtumbu na Mchenga.

2.2.6 Wanyama Pori na Jamii za Ndege

Orodha ya aina mbalimbali za wanyama pori na jamii mbalimbali za mimea zinazopatikana katika misitu hii ni pamoja na tembo, nyati, mbunju, kongoni, simba, nyumbu, pundamilia, mbalapi, swala, chui, mbango, nyani, ngedere, nguruwe, ngolombwe, ndope, ndandala, mbawala, paa, sungura, mbutuka, komba, njechele, kungusi, kikiu, mbuzi mawe, mnoda, nguchiro, mbawe, kima na Nungunungu.

Pia ndege wanaopatikana katika misitu hii ni ndege ngoma, kanga, kwale, chiriku, njiwa,tipitipi,kororo,njegea-msitu,kinjochi,kukunungu,pelepe, pondopondo,Ngulaka,Ngurukulu,Chengo,Bundi,Nalumbapala,Kwikwi na Mwewe.

2.3 Maeneo ya Usimamizi.

2.3.1 Msitu wa Mbumbila A

Msitu wa hifadhi wa Mbumbila A umegawanyika katika maeneo madogo Mawili ambayo ni eneo la uvunaji na eneo ambalo uvunaji hautafanyika.

Eneo lenye ukubwa wa hekta **51,475** sawa na **79.66%** ya msitu limetengwa kama eneo ambalo uvunaji hautafanyika ambapo kati ya hekta hizo **51,475** hekta **11,568** ni eneo ambalo limeathiriwa na shughuli za kilimo hivyo msitu unaanza kurudi katika hali yake baada ya wakulima kuhamishwa katika eneo hilo. Pia eneo lenye ukubwa wa hekta **33,445** ni eneo lenye mgogoro wa mpaka kati ya Nanjirinji A na Mirui ambapoUvunajiwa mazao ya Misitu hauruhusiwikabisa kwa sasa mpaka utatuzi wa mgogo ukamilike. Eneo lingine ambalo Uvunaji hautaruhisiwa ni eneo la asilimia kumi lenye ukubwa wa hekta **6462**.

Pia Msitu huu una maeneo ya Mabonde ambayo uvunaji hauruhusiwi kwa sababu ni hatari kwa wavunaji na pia endapo uvunaji utafanyika katika eneo hilo utasababisha mmomonyoko wa ardhi.

Eneo lenye ukubwa wa hekta **13,142 sawa na 20.34% ya msitu** ni eneo la uvunaji ambapo miti ya mbao yenye thamani imefanyiwa tathimini na kuandaliwa mpango wa uvunaji endelevu. Uvunaji endelevu wa miti iliyofanyiwa tathimini utafanyika katika eneo hili kwa kufuata mpango wa uvunaji ulioandaliwa.Maeneo ambayo yana asili ya

msitu ya ukanda wa pwani, yataruhusiwa kuvunwa lakini kwa utaratibu wa kutambua maeneo hayo kwa kuchukuchua alama za GPS (Misitu ya ukanda wa pwani ni misitu iliyofunga na isiyopukutisha majani kwa kipindi cha mwaka mzima na moto haiungui kwa sababu haina nyasi nyingi)

Maeneo yameonyeshwa katika kiambatisho B(i) kwenye ramani ya misitu ya Kijiji

2.3.2 Msitu wa Mbumbila B

Msitu wa hifadhi wa Mbumbila B umegawanyika katika maeneo madogo Mawili ambayo ni eneo la uvunaji na eneo ambalo uvunaji hautafanyika.

Eneo lenye ukubwa wa hekta 1,909 limetengwa kama eneo ambalo uvunaji hautafanyika.Uvunaji wa mazao ya Misitu hauruhusiwi kabisa katika eneo hili. Eneo hili limependekezwa kwa ajili ya ufugaji wa nyuki wa kisasa kwa sababu ufugaji huu ni rafiki wa mazingira na hauambatani na uvunaji wa Miti wala uchomaji wa moto. Pia eneo hili limechaguliwa kama eneo ambalo uvunaji haufanyiki kwa sababu lina uoto unao wakilisha hali ya Msitu mzima na ni makazi na mazalia ya wanyama zaidi ikiwa wanyama aina ya Nyani, Kima, mbawala,Paa,Mbutuka,mnoda,nguchiro,ndope,n.k.

Pia Msitu huu una maeneo ya Mabonde ambayo uvunaji hauruhusiwi kwa sababu ni hatari kwa wavunaji na pia endapo uvunaji utafanyika katika eneo hilo utasababisha mmomonyoko wa ardhi.

Asilimia **90** ya eneo lote la msitu sawa na hekta **17,078** ni eneo la uvunaji ambapo miti ya mbao yenye thamani itafanyiwa tathimini na kuandaliwa mpango wa uvunaji endelevu. Uvunaji endelevu wa miti itakayofanyiwa tathimini utafanyika katika eneo hili kwa kufuata mpango wa uvunaji ulioandaliwa. Eneo ambalo halipo katika asilimia kumi lakini lina asili ya msitu ya ukanda wa pwani, eneo hili litaruhusiwa kuvunwa lakini kwa utaratibu wa kutambua maeneo yaliyofanyiwa uvunaji kwa kuchukuchua alama za GPS (Misitu ya ukanda wa pwani ni misitu iliyofunga na isiyopukutisha majani kwa kipindi cha mwaka mzima na moto haiungui kwa sababu hauna nyasi nyingi)

Maeneo yameonyeshwa katika kiambatisho B(ii)kwenye ramani ya misitu ya Kijiji.

2.4 Matumizi ya Msitu

2.4.1 Mambo ya Asili & Haki za Kijadi

Hakuna matumizi yoyote ya kijadi ambayo hufanyika ndani ya misitu.

2.4.2 Historia ya Nyuma

Awali misitu hii ilikuwa inatumika kwa ajili ya kupata asali, kuwinda wanyama na uvunaji wa mbao holela kwa kiasi kikubwa.

2.4.3 Matumizi ya Sasa

Kwa sasa misitu hii inatumika kwa ajili ya shughuli za uvunaji magogo na mbao kiuendelevu, uwindishaji na ubanguaji wa asali. Misitu hii kwa sasa ni misitu ya hifadhi ya Kijiji ambapo Kamati ya Maliasili ndio meneja wa usimamizi wa Misitu. Matumizi ya sasa yatakayofanyika katika Misitu hii ya kijiji cha Nanjirinji A ni; *uvunaji endelevu, uhifadhi wa vyanzo vya maji na bionuwai na matumizi ya maza*o yasio timbao yanayofuata utaratibu ulio pangwa na Kijiji pamoja na uokotaji wa kuni.

SURA YA TATU

3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU.

Misitu itasimamiwa kama misitu ya asili na kutakuwa na mabadiliko kiasi katika usimamizi huo ili kuepuka kubadilisha hali ya uasilia wa misitu. Taratibu za kuingia misituni na za matumizi ya mazao ya misitu yameelezewa katika sheria ndogo za usimamizi wa misitu ya kijiji cha Nanjirinji A. Wale ambao hawatafuata taratibu hizi watapigwa faini kulingana na sheria ndogo za usimamizi wa misitu za kijiji cha Nanjirinji A.

3.1 Matumizi ya Msingi

Wanajamii wa kijiji cha Nanjirinji A watakuwa na haki ya kuingia katika Misitu wa Kijiji bila kibali na kupita njia zinazofahamika, haki hii itahusu vijiji jirani vya karibu. Wanajamii pia watakuwa na haki ya kuchota maji katika vyanzo vya maji vilivyopo katika misitu.

Wasio wakazi wa kijiji hawataruhusiwa katika maeneo ya kijadi bila uangalizi wa Kamati ya Maliasili.

3.2 Matumizi Huru ya Misitu

Matumizi huru kwa wanakijiji wa Nanjirinji A yatakuwa kwa ajili ya mazao yasiyotimbao kama vile uyoga, matundapori, mbogamwitu, kuni, nyasi na madawa ya asili. Vyote hivyo vitapatiwa kibali maalum cha bure toka Kamati ya Maliasili kwa kushirikiana na Hamashauri ya Kijiji. Wasio wakazi wa Kijiji cha Nanjirinji A wanaweza pia kuomba kibali toka Kamati ya Maliasili ya Kijiji kutumia mazao yaliyotajwa hapo juu. Kamati ya Maliasili itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mazao haya yanatumiwa kiendelevu. Watumiaji wa nje ya Kijiji wanaotaka kuvuna mazao haya kwa ajili ya biashara wanaweza kutozwa ushuru kama ilivyopangwa na Kamati ya Maliasili.

Kibali cha kutundika mizinga ya nyuki kitatolewa bure kwa kijiji cha Nanjirinji A.

3.3 Shughuli katika Misitu Zitakazotozwa Ushuru

Kutakuwa na ushuru wa Serikali ya Kijiji kwa shughuli zifuatazo kwenye misitu;

4 Kutembelea misitu kwa ajili ya mafunzo

5 Utafiti

6 Utalii kwenye misitu.

Viwango vya ushuru vimeonyeshwa katika Kiambatisho D. Wataalamu na wawezeshaji ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia kufanikisha kwa mpango huu hawatahusika na kutozwa ushuru.

3.4 Mazao Yanayohitaji Vibali vya Uvunaji

Kabla ya kuvuna jamii yeyote ya miti, lazima tathmini ifanyike ili kubaini kiasi kilichopo na mpango wa uvunaji utatayarishwa. Tathmini ya kina itafanyika kufuatana na mwongozo wa Tathmini Shirikishi ya rasilimali za misitu wa Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Taarifa za Tathmini shirikishi zimeambatanishwa katika mpango huu.Tathmini shirikishi haitafanyika katika eneo lililotengwa kwa ajili ya hifadhi (eneo la 10% la msitu).

Mpango wa uvunaji utaelezea namna kiwango cha uvunaji kilivyopatikana kutokana na matokeo ya tathmini na utabainisha ni kwa namna gani kiwango hicho ni endelevu.

Mpango wa uvunaji ni lazima uandaliwe na Kamati ya Maliasili, upitishwe na Mkutano Mkuu wa Kijiji na kuambatanishwa katika mpango huu.

Taarifa ya tathimini shirikishi ya MsituwaMbumbila A (hekta 13,142)

Kiasi cha Kuvuna Kiendelevu katika Msitu	**Miti ya Kati (Idadi)**	**Miti Mikubwa (Idadi)**	**Ujazo kwa Miaka Mitano (m^3)**	**Ujazo kwa Mwaka (m^3)**
Mpingo	684	295	912	182
Mpangapanga	1,083	0	1,880	376
Msenjele	2,466	69	3,375	675
Mlondondo	1,558	0	2,141	428
Mninga jangwa	448	0	667	133
Mkongo	303	0	819	164
Mkwaju	611	0	1,602	320
Mgongo	750	0	1,788	358
Mpupi	249	0	458	92
Msufi Pori	235	0	742	148
Mchenga	395	0	620	124
Mnidu	121	0	255	51
Mkunya	454	30	1,693	339
Mninga bonde	55	21	220	44
Mnepa	110	0	201	40
Mlipa deni	138	0	242	48
Mtumbitumbi	51	0	171	34

Taarifa ya tathmini shirikishi ya Msitu wa Mbumbila B(hekta 18,987)

Kiasi cha KuvunaKiendelevukatika Msitu	**Miti ya Kati (Idadi)**	**Miti MiKubwa (Idadi)**	**Kiasi cha Kuvuna Kiendelevu katika Msitu kwa Kipindi cha Miaka 5 (m3)**	**Kiasi cha Kuvuna Kiendelevu katika Msitu kwa mwaka (m3**
Mchenga	4,317	0	6,484	1,297
Mpingo	1,096	253	541	108
Msenjele	986	0	1165	233
Mlondondo	3,144	0	3,915	783
Mninga jangwa	2,517	0	3,457	691
Mninga bonde	106	0	199	40
Mkongo	252	0	565	113
Mgelegele	101	0	214	43
Mwembeti	391	0	885	177
Mpangapanga	142	0	259	52
Msufi pori	240	0	756	151
Mgongo	3,144	0	,7085	1,417
Miombo	31	0	36	7

Hakuna jamii yeyote ya miti itavunwa pasipo uendelevu, mbali na jamii za miti zilizoorodheshwa katika judwali hapo juu hakuna jamii yeyote ya miti itavunwa kwa biashara katika kipindi chote cha utekelezaji wa mpango. Kama Kijiji cha Nanjirinji A kitahitaji kuruhusu uvunaji wa jamii ambazo hazikuorodheshwa katika mpango huu, itabidi kijiji kiandike barua ya kumtaarifu Afisa Misitu wa Wilaya ili tathimini ifanyike na mpango wa uvunaji kwa ajili ya jamii hizo uandaliwe. Kabla ya kufanya uvunaji ni lazima Afisa Misitu wa Wilaya ajiridhishe.

3.4.1 Utaratibu wa Kupata Leseni ya Uvunaji Miti ya Mbao.

Utaratibu huu utahusisha miti yote iliyoorodheshwa katika kipengele 2.2.4juu au iliyofanyiwa tathimini na kuandaliwa mpango wa endelevu wa uvunaji.

1. Uvunaji utafanyika kwa kufuata Mwongozo wa uvunaji katika misitu ya vijiji wa mwaka 2015 uliotolewa na Wizara ya Malaisili na Utalii na Mwongozo wa Uvunaji wa Misitu ya Asili wa mwaka 2017 pia uliotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mtu yeyote anayetaka kuvuna mazao ya misitu toka Msitu wa Kijiji lazima kwanza aandike barua ya maombi kijijini na aonyeshe aina na kiasi anachotarajia kuvuna. Pia atajaza fomu ya Maombi ya uvunaji na lazima awe amekidhi mashariti ya Kuwa mfanyabiashara wa mazao ya Misitu kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za uvunaji.
2. Halmashauri ya Kijiji kwa kushirikiana na Kamati ya Maliasili itajadili na kupitisha ombi hilo endapo itaridhia kuwa maombi ya mteja yanakidhi matakwa ya mpango

wa uvunaji. Kama mpango wa uvunaji haujaandaliwa kibali hakitatolewa na uvunaji hauruhusiwi.

3. Halmashauri ya Kijiji kwa kushirikiana na Kamati ya Maliasili itapanga bei ya kuvuna mazao ya misitu na bei hizo kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji lakini bei itakayopangwa isiwe chini ya kiwango kilichowekwa na Serikali kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN) la kipindi husika .
4. Kamati ya Maliasili wakishirikiana na Serikali ya Kijiji pamoja na Afisa Misitu wa Wilaya watapanga bei ya mabaki yaliyoachwa kwenye Misitu baada ya uvunaji.
5. Kijiji na Mteja lazima waingie Mkataba wa kimaandishi kabla ya uvunaji kuanza
6. Mwombaji atalipia benki gharama za ujazo wa mti mzima uliosimama aliyoomba kwa Kamati ya Maliasili kupitia akaunti ya Kamati ya Maliasili na kupatiwa leseni yake pamoja na stakabadhi halali ya malipo.Kamati ya Maliasili itabaki na nakala moja ya kibali hiki.
7. Mwombaji atawasilisha nyaraka zake kwa Afisa Misitu wa Wilaya kwa uhakiki na akijiridhisha ataridhia uvunaji uanze.
8. Mwombaji atarudi tena Kijijini na kuwasilisha leseni iliyopata idhini ya Afisa Misitu wa Wilaya. Kamati ya Maliasili itamwonyesha eneo la kuvuna mazao ya misitu anayoyahitaji.
9. Baada ya kuvuna magogo yote yaliyokatwa na visiki yatagongwa nyundo ya Kijiji ili kuyahalalisha.
10. Mwisho mwombaji lazima apate kibali cha kusafirishia toka kwa Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ili aweze kusafirsha mazao yake bila usumbufu toka eneo moja kwenda eneo lingine.Mvunaji lazima awasilishwe kibali cha kusafirishia kwa Afisa Mtendaji wa kijiji na Kamati ya Maliasili ili kuweka kumbukumbu ya nambari ya kibali kabla mzigo haujatolewa kijijini.
11. Utaratibu huu utafuatwa kwa ununuzi wa mabaki ya magogo, vilingu na mazao mengine ya misitu yatakayovunwa kibiashara.
12. Kijiji hakitaruhusiwa kutoa leseni au vibali vya uwindaji wa Wanyamapori, vibali na leseni vitatolewa na Afisa Wanyamapori wa Wilaya au Serikali Kuu.

3.5 Matumizi Yasiyoruhusiwa ndani ya Msitu

- Kilimo ndani ya misitu.
- Kukata kuni mbichi
- Uchakataji wa mbao na magogo kwa kutumia chainsaw;
- Uvunaji katika maeneo ya 10% ya Misitu (Maeneo yasiyo ya uvunaj) au katika maeneo ya chanzo cha maji - mita sitini kutoka kingo za mto kama ilivyoainishwa katika kipengele 2.3 hapo juu;
- Malisho ya mifugo ndani ya misitu.
- Makazi ndani ya misitu.
- Uvunaji wa miti ya mbao ambayo haijaorodheshwa katika kipengele 2.2.4 juu au miti ambayo haijatengenezewa mpango wa uvunaji.
- Uvunaji katika maeneo muhimu ya kimila na jadi.
- Kuchoma moto ovyo.
- Uanzishwaji wa njia mpya zisizo rasmi ndani ya misitu.

- Uzalishaji mkaa.
- Uchimbaji mdogo wa madini.

SURA YA NNE

4: HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU

Misitu ya Kijiji cha Nanjirinji A ina wadau wafuatao; Serikali ya Kijiji, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Serikali Kuu na wadau wengine. Majukumu ya kila mdau yameelezewa kama ifuatavyo:

4.1 Kijiji

4.1.1 Haki

- Kumiliki na kutunza misitu ya Kijiji.
- Kukamata, kupiga faini au kumshitaki mtu yeyote anayeenda kinyume na sheria ndogo za kijiji zilizopitishwa pamoja na mpango huu.
- Kutumia rasilimali kama ilivyobainishwa katika mpango wa Usimamizi wa Misitu.
- Kukusanya na kutumia ushuru na mapato mengine yatokanayo na mazao ya misitu katika shughuli za maendeleo ya jamii na hivyo kuboresha hali za maisha ya wanajamii.
- Kufanya maamuzi juu ya usimamizi na matumizi ya misitu kwa kufuata sheria,sera na miongozo ya misitu.

4.1.2 Manufaa

- Kutumia mazao ya misitu bila mashariti magumu kama ilivyoainishwa katika mpango wa usimamizi shirikishi misitu.
- Kutumia miti na mbao kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa huduma za jamii Kijijini.
- Mapato yatokanayo na faini na ushuru wa mazao ya misitu yatakuwa ni mali ya Kijiji.
- Kupata mafunzo ya kitaalam katika masuala mbalimbali ya usimamizi misitu na kuboresha maisha ya jamii.

4.1.3 Majukumu ya Serikali ya Kijiji

- Msimamizi mkuu wa shughuli zote za utunzaji wa misitu.
- Kudhibiti mapato na matumizi yote yatokanayo na misitu.
- Kutatua migogoro inayohusiana na misitu pale inapojitokeza na kupeleka matatizo hayo ngazi ya Halmashauri ya Wilaya pale yanaposhindikana kutatua Kijijini.
- Kutunga, Kuboresha na Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo na Mpango wa Usimamizi wa Misitu ya Kijiji.
- Kuhakiki vibali vyote vilivyotolewa na Kamati ya Maliasili.
- Kupokea taarifa za uharibifu wa misitu toka Kamati ya Maliasili na wanakijiji kwa ujumla na kuzifanyia kazi.
- Kujadili na kupitisha bajeti na mipangokazi ya mwaka ya Misitu ya Kijiji iliyoandaliwa na kamati ya Maliasili.
- Kujadili na kuidhinisha mapendekezo ya matumizi yote ya fedha kwa Kamati ya Maliasili, doria na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya shughuli za misitu.
- Kutoa taarifa ya matatizo yanayohusiana na utunzaji wa Misitu katika Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) na Halmashauri ya Wilaya.

- Kushirikiana na wadau wengine katika utunzaji na usimamizi wa misitu.

4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili

Kamati ya Maliasili ina majukumu yafuatayo:

- Kuratibu shughuli zote za msitu kama vile; upandaji miti, ukusanyaji wa mazao ya misitu na kutunza kumbukumbu za misitu.
- Kutoa vibali vya uvunaji wa mazao ya misitu.
- Kuhakikisha doria imefanyika kila mara na kwa uhakika.
- Kuandaa mpango wa kazi wa mwaka wa shughuli za misitu.
- Kutathmini rasilimali za misitu na kutengeneza mpango wa uvunaji.
- Kutoa taarifa za maendeleo na uharibifu wa misitu kwa serikali ya kijiji.
- Kusimamia na kufuatilia uvunaji.
- Kuratibu shughuli zote zinazofanyika kwenye misitu.
- Kupendekeza na kusimamia sheria ndogo ikiwemo kuzirekebisha inapohitajika.
- Kuijulisha jamii juu ya matukio katika Misitu ya Kijiji na maeneo yanayozunguka.
- Kuielimisha jamii juu ya mabadiliko ya miongozo mbalimbali ya utunzaji misitu.
- Kutoa taarifa ya robo, nusu na mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa misitu kwa Halmashauri ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa Kijiji.
- Kuhamasisha ushiriki wa wanakijiji katika uhifadhi wa Misitu.
- Kufanya vikao vya Kamati ya Maliasili kila mwezi.
- Kujua mipaka ya Misitu na kuilinda.

4.1.4.1 Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili

- Kusimamia shughuli zote za Kamati ya Maliasili ikiwa ni pamoja na vikao
- Kuitisha mikutano ya Kamati ya Maliasili
- Kuwa msemaji mkuu wa Kamati ya Maliasili
- Kusaini Mihutasari yote ya vikao vya Kamati ya Maliasili
- Kuhakikisha kuwa Katibu anaweka kumbukumbu sahihi kuhusu vibali, mipango kazi, taarifa za mrejesho, mapato, doria na faini
- Kuhakikisha kuwa taarifa zinaifikia Serikali ya Kijiji
- Kutoa taarifa za mafanikio na matatizo ya ulinzi wa Misitu na shughuli zingine za Kamati Maliasili
- Atakuwa ni kiungo kati ya Kijiji chake na vijiji vingine vinavyopakana na Misitu na atawezesha ushirikiano kati ya Afisa Misitu wa Wilaya, wadau wengine wa maliasili na wanakijiji.

4.1.4.2 Katibu wa Kamati ya Maliasili

- Kuweka kumbukumbu za Kamati ya Maliasili
- Kuandaa agenda za mikutano
- Kuandika mihutasari ya vikao vinavyofanywa na Kamati ya Maliasili
- Kutoa taarifa za Kamati ya Maliasili kwenye Halmashauri/Serikali ya Kijiji
- Kutoa vibali vya uvunaji baada ya kupitishwa na Serikali ya Kijiji
- Kuratibu shughuli za doria
- Kuwaalika wajumbe kwenye mikutano baada ya kuwasiliana na Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili
- Kutekeleza shughuli nyingine zozote atakazo agizwa na Kamati ya Maliasili kupitia Mwenyekiti.

4.1.4.3 Muweka Hazina wa Kamati ya Maliasili

- Kutunza vitabu vya kumbukumbu vya fedha za Kamati ya Maliasili
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi kwa Kamati ya Mailiasili kila mwezi
- Kupokea mapato yanayotokana na mazao ya misitu na kutoa stakabadhi
- Kusaini stakabadhi na risiti zote zinazohusiana na malipo ya fedha.

4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji

- Kuzuia uharibifu wowote utakaojitokeza katika misitu kama vile uchomaji moto na uvunaji holela wa mazao ya misitu.
- Kutoa taarifa ya uharibifu wa aina yeyote utakaofanyika ndani ya msitu kwa Kamati ya Maliasili na Serikali ya Kijiji.
- Kushiriki katika shughuli zote za kuboresha misitu.
- Kupitia na kuidhinisha inapofaa sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili.
- Kushiriki katika kulinda misitu na kutoa msaada kwa timu ya doria mara kwa mara.
- Kupokea au kudai na kujadili taarifa zinazohusu maendeleleo ya Misitu, mapato na matumizi na baadae kupitisha au kutoa maelekezo kwa Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Maliasili
- Kupitia, kuboresha na kuidhinisha mpango wa usimamizi wa Misitu na sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili na Halmashauri ya Kijiji

4.2 Halmashauri ya Wilaya

4.2.1 Haki

- Kupokea taarifa za mwezi, robo na nusu mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa misitu.
- Kukagua vitabu vya mapato na matumizi na kuchukua hatua zinazotakiwa kama italazimu.
- Kurudisha mamlaka ya usimamizi wa misitu chini ya Halmashauri ya Wilaya kama Kijiji kitashindwa kuusimamia ipasavyo.

4.2.2 Manufaa

- Kupungua kwa gharama za usimamizi wa misitu.

- Kuboreka kwa usimamizi wa misitu.
- Kupungua kwa migogoro na migongano inayohusiana na matumizi ya misitu kati ya Halmashauri ya Wilaya na jamii.
- Kuboreka kwa usimamizi wa misitu na hivyo kudhibiti ufyekaji wa Misitu na kupunguza uharibifu wa Misitu;

4.2.3 Majukumu

- Kupitisha Mpango wa Usimamizi Misitu, Sheria ndogo na Mpango wa uvunaji.
- Kuhalalisha mazao yatokanayo na Misitu ya Kijiji.
- Kutoa wataalamu kwa ajili ya shughuli za misitu pale inapohitajika.
- Kusaidia kutafuta soko la mazao ya Misitu.
- Kusimamia na kutatua migogoro ambayo iko juu ya uwezo wa Serikali ya Kijiji.
- Kuongoza zoezi la kubaini fursa na vikwazo katika kipindi cha kwanza na cha mwisho cha mpango huu.
- Kuingilia kati kama kuna jambo au shughuli yeyote imefanyika kinyume cha utaratibu wa mpango kazi.
- Kufuatilia na kushauri au kuchukua hatua wakati wote wa utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa Misitu na mipango ya uvunaji ya Misitu;
- Kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na Misitu yanatumika vizuri na Kijiji kama ilivyopitishwa na Mkutano mkuu wa Kijiji.

4.3 Serikali Kuu

4.3.1 Majukumu

- Kutoa wataalamu washauri pale wanapohitajika.
- Kutunga Sheria, Sera na kutoa miongozo mbalimbali inayohusu usimamizi misitu.

4.4 Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's)

4.41 Majukumu

- Kutafuta masoko ya mazao ya Misitu
- Kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa Misitu
- Kutoa msaada wa kitaalamu na kusaidia uendeshaji wa shughuli za kuendesha Misitu
- Kuwezesha kufanya tathimini za rasilimali za Misitu pale itakapohitajika
- Kufuatilia na kutoa ushauri wa utekelezaji wa shughuli za kuendeleza Misitu

5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU

Mambo yatakayoangaliwa ni pamoja na upandaji wa miti na utunzaji wa machipukizi dhidi ya moto, ulinzi wa misitu, kinga na udhibiti wa moto pamoja na mipango ya muda mrefu ya matumizi endelevu wa mazao ya misitu. Mwongozo wa mpango wa utekelezaji wa miaka mitano umeonyeshwa katika kiambatisho B.

5.1 Mikakati ya Jumla ya Kuendeleza Msitu

Katika kuendeleza misitu, mikakati ifuatayo imewekwa;

- Kudhibiti uchomaji moto ovyo kwenye misitu
- Kudhibiti malisho ya mifugo kwenye misitu
- Kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti uvunaji holela na uharibifu mwingine wa misitu
- Kusafisha mipaka ya misitu
- Kuelimsha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza Misitu
- Kuweka alama za kudumu kwenye mipaka ya Misitu mfano kupaka misitu rangi na kuweka mabango
- Ubabuaji moto wa Misitu
- Kuhamasisha jamii kupanda miti
- Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo na mpango wa usimamizi wa Misitu (Serikali ya Kijiji)
- Kukusanya mapato yanayotokana na Misitu (Kamati ya Maliasili)
- Kununua vitendea kazi vya Kamati ya Maliasili
- Kukuza ushirikiano na Vijiji vingine juu ya uhifadhi wa Misitu
- Kuweka mpango mzuri wa Kamati mpya kuwa na uwakilishi wa Kamati ya zamani
- Kuwezesha urahisi wa mawasiliano kwa wadau wote ili kupiga vita vitendo vya uharibifu wa Misitu
- Kijiji kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi na upatikanaji wa pembejeo za kilimo ili kupunguza kasi ya kilimo cha kuhamahama
- Kuandaa na kutoa taarifa ya mwaka
- Kufanya mapitio ya mpango wa usimamizi wa Misitu

5.2 Ulinzi wa Misitu

Usimamizi wa Misitu ya Kijiji utakuwa chini ya serikali ya kijiji na utatunzwa na wanajamii.

5.2.1 Ushirikishwaji wa Jamii katika Ulinzi wa Misitu

Misitu italindwa na wanajamii wote wanaozunguka na wanaopakana na misitu. Kila mtu atatoa taarifa kwa uongozi wa kijiji au kamati ya maliasili au kikosi cha doria pale

anapoona uharibifu katika misitu. Kamati ya maliasili itaratibu na kusimamia shughuli za doria.

5.2.2 Walinzi wa Doria

Kutakuwa na timu ya doria itakayochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji ambayo itakuwa na jukumu la kufanya doria za mara kwa mara katika misitu ya jamii. Kikosi cha doria kitakuwa na wajumbe wafuatao:-

- Kamanda mmoja wa kikosi
- Wajumbe watatu wa Kamati ya Maliasili.
- Wanajamii wawili wenye uelewa wa masuala ya misitu

Doria inaweza kuwa ya wanakikosi wanne hadi sita, na kila doria lazima awepo mjumbe mmoja wa kamati ya maliasili, na mwanajamii mmoja. Kikosi cha doria kitaweka kumbukumbu zote za doria katika kitabu cha doria na kitatoa taarifa za matukio kwa Kamati ya Maliasili baada ya doria. Doria itafanyika angalau mara mbili kwa mwezi kwa kila msitu. Wanadoria watalipwa posho endapo kuna fedha na kutokana na bajeti ya Kamati ya Maliasili iliyopitishwa na Halmashauri ya Kijiji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

Kikosi cha doria kitachaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji. Kamanda wa kikosi cha doria atakuwa na sifa zifuatazo; mtu shupavu ambaye ni mwaminifu,Awe amefuzu mafunzo ya mgambo,Ambaye ana moyo wa kujituma na kjitolea na Awe anafahamu vizuri maeneo ya Misitu. Wanakikosi watabadilishwa na mkutano mkuu wa kijiji kila baada ya miezi sita au wakati wowote inapobidi kufanya hivyo.

Wanakikosi cha doria watakaobainika kutokuwa waaminifu watafukuzwa mara moja na wengine watachaguliwa kujaza nafasi zao.

5.3 Kusafisha Mipaka na Barabara za Moto

Kamati ya Maliasili ya kijiji na jamii kwa ujumla watashiriki katika kusafisha mipaka ya misitu na kutengeneza barabara za moto. Kamati ya Maliasili itaamua wapi barabara za moto zipite baada ya kupata ushauri toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya. Ubabuaji moto ni hatua mojawapo muhimu katika kudhibiti moto, na hili ni jukumu la kamati ya maliasili na wanajamii kwa ujumla. Zoezi la ubabuaji na usafishaji wa barabara za moto ni kazi ngumu inayohitaji fedha toka vyanzo mbalimbali. Kamati ya Maliasili ya Kijiji na jamii kwa ujumla watashiriki katika kuandaa mpango wa kudhibiti mioto kwenye Misitu. Ubabuaji moto ni hatua mojawapo muhimu katika kudhibiti moto, na hili ni jukumu la Kamati ya Maliasili na wanajamii kwa ujumla. Zoezi la ubabuaji litatekelezwa na wanajamii wote kwa usimamizi wa Afisa misitu au wataalamu wa moto.

5.4 Kurudisha hali ya Misitu

5.4.1 Kutokana na Machipukizi (Uoto wa asili)

Njia hii hutegemea miche iliyoota yenyewe kutokana na mbegu, mashina au mizizi ya miti iliyovunwa.

5.4.2 Upandaji wa miti kwenye maeneo yaliyo wazi

Maeneo yote yaliyo wazi ndani ya msitu ambayo yanaonekana ni vigumu uoto wa asili kujaza yatapandwa miti inayokubaliana na mazingira hayo hasa ile iliyokuwepo lakini

ikaadimika kutokana na matukio ya moto ya mara kwa mara na uvunaji holela uliokuwa ukifanyika kipindi cha nyuma.

5.4.3 Palizi kwenye maeneo yaliyopandwa miti

Palizi ya kisahani itafanyika mara moja kwa mwaka ili kuhakisha miche iliyopandwa haisongwi na majani au mimea mingine.

SURA YA SITA

6: MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU

6.1 Vyanzo vya Mapato

Kutakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo toka misitu ya jamii:

- Ushuru
- Ada za leseni
- Ada za vikundi vilivyoko mafunzoni, shughuli za utafiti na utalii
- Faini za wahalifu
- Mauzo ya rasilimali za Misitu

6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau

1. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa asilimia tano (5%).

2. Serikali ya Kijiji asilimia hamsini (50%).

3. Kamati ya Maliasili asilimia arobaini (45%).

MUHIMU:

Mapato yatakayotolewa leseni kama vile mbao,magogo na **vilingu** ndio

yatakayogawanywa.

6.3 Matumizi ya Mapato

Mapato yatokanayo na misitu yataelekezwa katika shughuli za;

- Kuendeleza shughuli za misitu zilizopangwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Mapato yatakayobaki yatapelekwa kwa serikali ya kijiji ili yatumike katika shughuli za jamii.
- Kulipa motisha (posho) kwa doria.
- Ununuzi wa vifaa muhimu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za misitu kama ilivyobainishwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Matumizi mengine ya ziada ya kuendeleza misitu yaliyoidhinishwa na Serikali ya Kijiji.
- Ununuzi wa vitabu kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za shughuli za misitu.
- Kuchangia katika shughuli za maendeleo kijijini.

6.4 Ukusanyaji na Utunzaji wa Fedha

Fedha zote zitatunzwa benki isipokuwa kwa fedha chache kwa ajili ya matumizi madogodogo. Pesa ndogondogo haitakiwi kuzidi shilingi 2,000,000/-. Kutakuwa na akaunti benki itakayofunguliwa kwa jina la Kamati ya maliasili Nanjirinji A Kutakuwa na watia sahihi wanne; Afisa Mtendaji wa Kijiji (A), Mjumbe mmoja wa Kamati ya Mipango ya Kijiji (A), Mwenyekiti (B) na mweka Hazina (B) wa Kamati ya Maliasili ya kijiji. Mtia sahihi mmoja wa A na mmoja wa B watahitajika kuchukua pesa toka benki.

6.4.1 Vitabu Muhimu vya Kutunza Kumbukumbu Vinavyotakiwa

Mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili atakuwa na jukumu la kutunza vitabu vya kumbukumbu. Vitabu vinatakiwa kuwa tayari kwa ukaguzi wakati wowote na vitakaguliwa na;

- Kamati ya fedha na mipango ya serikali ya kijiji.
- Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya.

Vitabu vitakavyokaguliwa ni;

- Jalada la kumbukumbu/muhitasari wa vikao.
- Kitabu cha kumbukumbu za doria kinachoonyesha tarehe ya doria, njia iliyotumika, kama kuna wahalifu waliokamatwa na dalili zozote za kuwepo kwa uharibifu wa msitu.
- Kitabu cha kumbukumbu za uhalifu kinachoonyesha majina ya wahalifu, faini zilizolipwa, tarehe na nambari ya stakabadhi.
- Vitabu vya vibali na leseni vinavyoonyesha nambari ya kibali, mpewaji, sababu ya kibali, kiasi cha mzigo, kiasi cha fedha, nambari ya stakabadhi, tarehe na jina la mwanakamati aliyesimamia.
- Kitabu cha stakabadhi za malipo yote yaliyofanyika kulingana na mpango kazi huu.
- Kitabu cha matumizi madogo madogo kwa ajili ya kumbukumbu za matumizi ya pesa ambazo hazikuwekwa katika akaunti ya benki.

6.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi

Kamati ya Maliasili itatoa taarifa ya Mapato na Matumizi kila mwezi kwa Serikali ya Kijiji. Pia kila baada ya miezi mitatu Serikali ya Kijiji itatoa taarifa za Kamati ya Maliasili katika mkutano mkuu wa kijiji ambapo Kamati ya Maliasili nayo inaweza kuwakilisha taarifa.

6.4.3 Kuwajibishwa

Mwanakamati au mwanakijiji yeyote atakayepatikana na kosa la kutumia vibaya fedha zilizotokana na Misitu atawajibishwa na Serikaliya Kijiji au atashitakiwa katika Baraza la usuluhishi la Kata au Mahakama ya mwanzo kwa kupata ushauri kutoka kwa Afisa

Mtendaji wa Kata au Afisa Misitu wa Wilaya. Mjumbe yeyote wa Serikali ya kijiji au Kamati ya Maliasili atakayepatikana na kosa lazima awajibishwe kulingana na Sheria ndogo za usimamizi wa Misitu za kijiji na ikilazimika ajiuzulu au atalazimishwa kujiuzulu haraka na uchaguzi mpya utafanyika kumchagua mjumbe mwingine kuziba pengo hilo.

SURA YA SABA

7: UFUATILIAJI NA TATHIMINI

7.1 Ufuatiliaji

Serikali ya Kijiji itafuatilia shughuli zote zilizopangwa kulingana na mpango kazi wa kila mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli zote zimefanyika kulingana na mpango kazi.

7.2 Tathimini ya Kati na ya Mwisho

Zoezi la kubaini fursa na vikwazo litafanyika ili kuelewa hali ya maendeleo kama ilivyobainishwa katika mpango kazi huu. Zoezi hili litafanyika mwishoni mwa mwaka wa pili, na mwishoni mwa kipindi cha miaka mitano.

Tathimini itafanyika kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la utekelezaji wa mpango kazi lililoonyeshwa katika kiambatisho C. Zoezi hili la tathmini litaongozwa na Afisa Misitu wa Wilaya chini ya mpango wa kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu.

UHALALI WA MPANGO

Mpango wa Usimamizi Misitu

Mpango huu wa Usimamizi Misitu wa Kijiji cha Nanjirinji A umepitishwa na mkutano mkuu wa kijiji na kuidhinishwa na Afisa Misitu wa Wilaya. Sheria ndogo zilizoambatanishwa na mpango huu zimepitishwa na Mkutano mkuu wa Kijiji, Baraza la maendeleo la Kata na Baraza la madiwani.

Mpango huu unasisitiza kuwa ni jukumu la wanakijiji wa Nanjirinji Akutunza, kusimamia, kutumia kiendelevu na kuendeleza msitu wao kufuatana na malengo ya mpango wa Usimamizi msitu.

Marekebisho ya Mpango

Jamii ya kijiji cha Nanjirinji A itafanya marekebisho ya jambo lolote katika mpango huu, wataomba ushauri kwa Afisa Misitu wa Wilaya ambaye atashauri na kutoa maoni juu ya marekebisho hayo. Marekebisho hayo yakikubaliwa yatatiwa saini na yataambatanishwa katika mpango huu. Kwa madhumuni ya ufanisi wa haraka wa marekebisho hayo, Afisa misitu wa Wilaya anaweza kutia sahihi kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya.

Mpango huu wa usimamizi wa msitu wa kijiji cha Nanjirinji Aumesainiwa na:

_____

Mwenyekiti wa Kijiji

_____

Mwenyekiti Kamati ya Maliasili

_____

Afisa Misitu wa Wilaya

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A : RAMANI INAYOONYESHA MIPAKA YA KIJIJI



Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Kijiji cha Nanjirinji A. Vijiji vinavyopakana na Nanjirinji A vimeonyeshwa, mawe ya mipaka yameonyeshwa kwa alama ya pembetatu na kupewa nambari. Vipimo vya GPS (UTM37L : WGS84) katika mawe ya mipaka ni kama ifuatavyo;

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
1		460235	8944693
2		489197	8955881
3		503638	8953739
4		512367	8930728
5		512049	8927395
6		468963	8902281
7		460631	8920769

KIAMBATISHO B : RAMANI INAYOONYESHA MIPAKA YA MISITU YA KIJIJI

i. Ramani inayoonyesha Mipaka ya Misitu wa Kijiji –Mbumbila A.



ii. Ramani inayoonyesha Mipaka ya Misitu wa Kijiji –Mbumbila B



Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Misitu wa Kijiji cha Nanjirinji A. Vipimo vya GPS (UTM37L : WGS84) katika mawe ya mipaka ni kama ifuatavyo;

MBUMBILA A

Namba	E (m)	N (m)
1	463577	8913287
2	463548	8938190
3	472431	8938622
4	469874	8935069

Namba	E (m)	N (m)
5	474115	8926166
6	484435	8928347
7	490809	8920675
8	491778	8918848
9	491031	8918247
10	477314	8906824
11	477303	8906802
12	472570	8905498
13	469607	8903263
14	468183	8904298
15	463577	8913287

MBUMBILA B

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
1.		470593	8944817
2.		505453	8950846
3.		500763	8948594
4.		495830	8945091
5.		496765	8943378
6.		495435	8943874
7.		491608	8947383
8.		483897	8943916
9.		478596	8942176
10.		475781	8942057
11.		473341	8939284
12.		472758	8938380
13.		471935	8938206
14.		466924	8938014
15.		464931	8943561
16.		465492	8944364
17.		466831	8944912

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
18.		470289	8944794

KIAMBATISHO C : MPANGO WA UTEKELEZAJI

Kila mwaka kamati ya maliasili ya kijiji ni lazima iandae mpango kazi kwa mwaka unaofuata.

Kazi za Kila Mwaka

- Doria za mara kwa mara
- Ubabuaji moto misitu
- Kuhamasisha jamii kupanda miti
- Kusimamia matumizi ya sheria ndogo (Serikali ya Kijiji)
- Kuweka kinga za moto (Kamati ya maliasili)
- Kuweka barabara za moto (Wanajamii/Kamati ya Maliasili)
- Ulinzi wa Misitu (jamii nzima)
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)
- Kukuza ushirikiano na vijiji vingine juu ya usimamizi wa Misitu
- Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza Misitu
- Kushirikisha vijiji jirani kwenye ulinzi wa Misitu

Kazi za Mwaka wa Kwanza

- Kubabua moto au kusafisha mipaka kuzunguka misitu (Jamii na Kamati ya maliasili)
- Kujenga kituo cha ukaguzi wa mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)
- Doria za mara kwa mara
- Kusimamia matumizi ya sheria ndogo (Serikali ya Kijiji)
- Kuweka kinga za moto (Kamati ya maliasili)
- Ulinzi wa Misitu (jamii nzima)
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)
- Kuweka mabango ya kupiga vita vitendo haramu na kuonyesha misitu.

Kazi za Mwaka wa Pili

- Doria za mara kwa mara
- Ubabuaji moto misitu
- Kusimamia matumizi ya sheria ndogo (Serikali ya Kijiji)
- Kuweka kinga za moto (Kamati ya maliasili)
- Kuweka barabara za moto (Wanajamii/Kamati ya Maliasili)

- Ulinzi wa Misitu (jamii nzima)
- Kupanda miti kwa maeneo ya mipaka na maeneo yaliyo wazi
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu (Kamati ya maliasili

Kazi za Mwaka wa Tatu

- ……

Kazi za Mwaka wa Nne

- ……..

Kazi za Mwaka wa Tano

…….

KIAMBATISHO D : VIWANGO VYA USHURU

Shughuli zifuatazo zitatozwa ushuru kwa Serikali ya Kijiji kwa kufuata Sheria ndogo za Kijiji kama ifuatavyo;

- Kufanya mafunzo ndani ya misitu kwa wageni kutoka nje ya nchi ni shilingi zisizopungua 150,000/= kwa kundi lisilozidi watu 20 kwa kila siku, na kwa wageni wa ndani ni shilingi zisizopungua 100,000/= zitalipwa kwa kundi lisilozidi watu 20 kwa kila siku. Wanafunzi wa shule za msingi na Sekondari hawatatozwa ushuru, wataruhusiwa kufanya mafunzo ndani ya misitu bure.
- Kufanya utafiti, ada itakayolipwa ni shilingi zisizopungua 15,000/= kwa siku kwa kila mtu mmoja na nakala ya taarifa ya utafiti itolewe kijijini, watakaowaongoza watalipwa kiasi kisichopungua 10,000/= kwa siku kwa kila mwongozaji mmoja.
- Wageni wanaotembelea kijijini kwa lengo la kufadhili shughuli za maendeleo hawatatozwa ushuru wowote.
- Kufanya utalii ndani ya msitu ni shilingi zisizopungua 20,000/= kwa kila mgeni kutoka nje ya nchi, Waongozaji watalipwa kiasi kisichopungua Shs. 10,000/= kila mmoja kwa siku moja. Wageni wa ndani ni Shilingi zisizopungua 2,000/= kwa kila mtalii mmoja. Waongozaji watalipwa kiasi kisichopungua Shs. 10,000/= kila mmoja kwa siku moja.
- Ushuru kwa kila lita moja ya asali ni shilingi 500/=.

KIAMBATISHO D: SHERIA NDOGO

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA ZA WILAYA

(SURA 287)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 168

SHERIA NDOGO ZA KUTUNZA NA KUSIMAMIA RASILIMALI ZA MSITU WA HIFADHI WA KIJIJI CHA NANJIRINJI A

Jina la Sheria 1 Sheria hizi zitaitwa sheria ndogo za kutunza, kusimamia na kutumia Rasilimali za misitu ya kijiji cha Nanjirinji A.

Tarehe ya kuanza kutumika 2 Sheria hizi zitaanza kutumika tarehe ***10*** mwezi ***6*** mwaka ***2018*** siku mbayo zimepitishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Kilwa

Tafsiri 3 **"Msitu wa kijiji**''maana yake ni eneo la msitu lililotengwa na Kijiji lenye miti na uoto mwingine wa asili linalomilikiwa na Kijiji cha Nanjirinji A.

"Mpango wa Usimamizi wa Misitu"maana yake ni kabrasha lenye maelezo ya namna jamii ya kijiji cha Nanjirinji A kitakavyo kuwa kina tunza, kusimamia na kutumia rasilimali za misitu.

"Halmashauri ya kijiji" maana yake wajumbe wasiopungua 15 na wasiozidi 25 wa Halmashauri ya Kijiji, kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982.

"Mkutano Mkuu wa kijiji"maana yake ni mkutano wa

Wananchi wote wa Kijiji cha Nanjirinji A, wenye Mamlaka na maamuzi ya mwisho katika kijiji cha Nanjirinji A. Ni kikao cha Kijiji kinachohudhuriwa na Wanakijiji wote wenye akili timamu na wenye umri usiopungua miaka 18.

"Kamati ya Maliasili ya Kijiji"Maana yake ni kamati iliyochaguliwa na kuundwa na Serikali ya Kijiji na kupitishwa na

Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Nanjirinji A ambayo majukumu yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu misitu iliyopo ndani ya mipaka ya kijiji na maliasili nyingine zilizomo kwenye kijiji cha Nanjirinji A.

"Meneja wa misitu"maana yake ni Kamati ya Maliasili ambayo kazi yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu Misitu ya Kijiji cha Nanjirinji A.

"Mwanakijiji"Maana yake ni mtu yeyote aliyeandikishwa kwenye orodha ya wakazi wa Kijiji na pia anatambulika na Serikali ya Kijiji cha Nanjirinji A kuwa mwanakijiji wa kijiji cha Nanjirinji A

"Kijiji"maana yake ni Kijiji cha Nanjirinji A pamoja na Vitongoji vyake.

"Kiongozi"Mtu yeyote aliyepewa madaraka na mamlaka na kijiji ili awatumikie

"Mazao ya Misitu" Maana yake ni rasilimali zote zinazotoka kwenye misitu kama vile mbao, magogo,mianzi, majengo, fito, asali, uyoga, matundapori, mbogamboga, kuni, Nyasi, madawa ya asili, kamba, viazi pori, ukindu na miyaa.

"**Madini**" maana yake ni madini ya vito, shaba, almasi, na ni pamoja na madini ya ujenzi ambayo ni mawe, kokoto, mchanga na kifusi; kama ilivyoainishwa katika sheria ya Madini ya mwaka 2010

"**Mkurugenzi**" ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa pamoja na mtu yeyote aliyeidhinishwa kufanya kazi kwa niaba ya Mkurugenzi, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, (Mamlaka za wilaya) ya mwaka 1982

"**Sheria**"- Maana yake ni sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tamko, mwongozo au kanuni yoyote iliyotolewa na serikali na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali

Utaratibu wa jumla wa kutumia Misitu na mazao ya

4 **UTARATIBU WA JUMLA WA KUTUMIA MISITU NA MAZAO YA MISITU**

I. Sheria ndogo hizi zitatumika kusimamia misitu yote ya kijiji

Misitu

na mingine itakayotengwa chini ya mpango wa usimamizi shirikishi.

II. Watu ambao wanaruhusiwa kuingia katika misitu ya kijiji kwa shughuli mbalimbali za usimamizi kutokana na taratibu zilizokubalika ni wakazi wa Kijiji cha Nanjirinji A tu.

III. Watu wengine kutoka nje ya kijiji cha Nanjirinji A wataruhusiwa Kuingia ndani ya Misitu ya Kijiji kwa vibali maalum na endapo watakuwa na shughuli iliyokubalika.

IV. Kwa wale wanakijiji wasiojiweza ambao wanatambuliwa na Serikali ya Kijiji kama vile wagonjwa wa kudumu, Walemavu na Wazee watachukua mazao ya msitu yasiyo ya biashara bure bila kutozwa ushuru wa aina yeyote.

V. Kwa mazao yasiyo ya biashara ambayo ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kama vile uyoga, matundapori, mbogamboga, kuni, Madawa na ukindu hapatakuwa na malipo ila kutakuwa na siku Maalum itakayo pangwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji ya kukusanya mazao hayo, siku hiyo inaweza kubadilika kutokana na matakwa ya jamii.

VI. Wanajamii wote wa Kijiji cha Nanjirinji A watakaohitaji mbao kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya kulala watalipia asilimia hamsini (50%) ya gharama ya bei iliyoelekezwa na Serikali. Fursa hiyo ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kulala Kijijini Nanjirinji A tu.Mwanakijiji atakaguliwa na uongozi wa kijiji kabla ya kibali kutolewa.

Uvunaji wa mazao ya Misitu kibiashara

5 UVUNAJI WA MAZAO YA MISITU KWA AJILI YA BIASHARA

Mazao yote ambayo ni kwa ajili ya biashara yatavunwa kwa kulipia ushuru na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002**.**

Masharti ya matumizi ya Misitu na mazao ya Misitu ya kijiji

6 **MASHARTI YA MATUMIZI YA MISITU NA MAZAO YA MISITU YA KIJIJI**

Bila kuathiri masharti mengine yaliyotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi matumizi ya Misitu na mazao ya Misitu ya Nanjirinji A yatakuwa kama ifuatavyo:-

i. **Matumizi yaliyoruhusiwa bila kibali wala ushuru ni:-**

   a. Kuchota maji kama kutakuwa na ulazima.

   b. Njia za miguu na barabara za kukatiza Misitu kama kutakuwa na ulazima.

ii. Matumizi yaliyoruhusiwa kwa vibali maalum bila malipo

ni kwa matumizi ya nyumbani kwa wakazi wa Nanjirinji A:-

a. Kukusanya matundapori, mbogamwitu,uyoga, kuokota kuni (miti mikavu tu), kukata miyaa, kuchimba viazi pori,upekecho, mawe ya kusaga na mianzi

b. Kutumia mazao ya Misitu kwa ajili ya maendeleo ya huduma za jamii

c. Kutundika Mizinga ya Nyuki.

iii. Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kulipiwa vibali au leseni

a. Kuvuna miti ya majengo kwa ajili ya biashara;

b. Kuvuna mbao na magogo.

c. Kukusanya vilingu/mabaki.

iv. Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kulipiwa ushuru/ada

a. Utafiti;

b. Utalii;

c. Urinaji wa asali kwa watu binafsi au vikundi visivyo vya Kijiji

d. Mafunzo ya vikundi.

Bila kuathiri kifungu kidogo cha (iii) (a,b na c) hapo juu utaratibu wa kuvuna magogo na mbao ni ule uliowekwa na Sheria ya Misitu.

v. Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya Misitu

a. Kuchoma moto ovyo Misitu ;

b. Kukata na kupasua miti ambayo haikuorodheshwa kwenye Mpango wala kufanyiwa tathmini;

c. Kutega wanyama pori;

d. Kuharibu uoto wa asili sehemu yeyote katika Misitu;

e. Kurina asali kwa kutumia moto;

f. Shughuli za kilimo,Makazi ya watu;

g. Kuchoma mkaa bila kufuata utaratibu uliokubaliwa na Kijiji;

h. Kuchunga mifugo;

i. Kurina asali kwa kuangusha miti kunakojulikana kama kubangua asali.

j.Kuchuna kamba kwenye miti iliyo ndani ya Misitu ya Kijiji.

MUHIMU:

a)Mtu yeyote atakayethibitika kuvunja sheria hii atatozwa faini isiyozidi 50,000/-pamoja na fidia ya uharibifu akishindwa kulipa

atapelekwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha miezi sita (6) kwenda jela.

b) Ni marufuku kuchana mbao kwa kutumia mashine ya mnyororo(chainsaw). Mashine ya mnyororo(chainsaw) itakayokamatwa katika shughuli za uharibifu wa mazao ya misitu itataifishwa na kupelekwa kwa afisa misitu wa Wilaya ya Kilwa.

(v) Matumizi mengine na Ushuru.

(i) Kufanya mafunzo ndani ya misitu kwa wageni kutoka nje ya nchi ni shilingi zisizopungua 150,000/= kwa kundi lisilozidi watu 20 kwa kila siku, na kwa wageni wa ndani ni shilingi zisizopungua 100,000/= zitalipwa kwa kundi lisilozidi watu 20 kwa kila siku. Wanafunzi wa shule za msingi na Sekondari hawatatozwa ushuru, wataruhusiwa kufanya mafunzo ndani ya misitu bure.

(ii) Kufanya utafiti, ada itakayolipwa ni shilingi zisizopungua 15,000/= kwa siku kwa kila mtu mmoja na nakala ya taarifa ya utafiti itolewe kijijini, watakaowaongoza watalipwa kiasi kisichopungua 10,000/= kwa siku kwa kila mwongozaji mmoja.

(iii) Kufanya utalii ndani ya misitu ni shilingi zisizopungua 20,000/= kwa kila mgeni kutoka nje ya nchi, Waongozaji watalipwa kiasi kisichopungua Shs. 10,000/= kila mmoja kwa siku moja. Wageni wa ndani ni Shilingi zisizopungua 2,000/= kwa kila mtalii mmoja. Waongozaji watalipwa kiasi kisichopungua Shs. 10,000/= kila mmoja kwa siku moja.

(iv) Wageni wanaotembelea kijijini kwa lengo la kufadhili shughuli za maendeleo hawatatozwa ushuru wowote.

(v) Ushuru kwa kila lita moja ya asali ni shilingi 500/=.

7

UTARATIBU WA UTEKELEZAJI

i. Litakuwa ni jukumu la Kijiji kutoza faini, kutoa vibali na kutoa uamuzi kwa shughuli zote zinazohusu sheria ndogo hizi. Halmashauri ya Kijiji inaweza kuagiza baadhi au shughuli zote hizi kwa Kamati ya Maliasili ya kijiji au ikibidi kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji, Kamati au Afisa Mtendaji aliyeagizwa atawajibika kwa Halmashauri ya Kijiji ambayo nayo itawajibika kwa Mkutano mkuu wa Kijiji.

ii. Vibali vyote vitatolewa na Kamati ya Maliasili na kukaguliwa na Halmashauri ya Kijiji. Lazima kibali kiwe na mhuri wa Serikali ya Kijiji pia kieleze mahali na muda mazao yatakapovunwa, idadi au kiasi na aina ya mazao hayo. Baada ya mazao kuvunwa, kupimwa, nakala moja ya kibali itabaki ofisi ya Serikali ya Kijiji.

iii. Kamati ya Maliasili kitaalam ndiyo Meneja wa usimamizi

wa Misitu . Kamati hii itadumu madarakani kwa muda wa miaka mitatu (3). Hata hivyo wajumbe wa kamati wanaweza kusitishwa na kukoma kuwa wajumbe endapo wataonekana kutofuata maadili ya Kamati ya Maliasili.Kamati ya Maliasili kiutendaji imeanza kazi mwezi wa 4 mwaka 2018.Angalau nusu ya wajumbe waliofanya vizuri katika kipindi hicho cha miaka mitatu watabaki katika Kamati kwa ajili ya kuwapa uzoefu wajumbe wapya waliochaguliwa.

iv. Wajumbe wa Kamati ya Maliasili watateuliwa au kubadilishwa na Halmashauri ya Kijiji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

v. Mwanakijiji/Wanakiji watakaofanikisha kupatikana kwa mzigo wa mbao kuanzia 50 atalipwa na kijiji shilingi 100,000/=.

vi. Lazima itolewe stakabadhi kwa ada zote, faini na mali zote zitakazotaifishwa.

vii. Kiongozi au mwanakijiji yeyote wa Kijiji cha Nanjirinji A anayo mamlaka ya kumkamata mtu yeyote anayefanya kosa kinyume na sheria ndogo hizi na kumfikisha katika Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Maliasili.

viii. Ni wajibu wa kila mwanakijiji kutoa taarifa ya ukiukwaji wa sheria hizi kwa uongozi wa Kijiji.

ix. Shughuli zote za kutunza, kusimamia na kutumia Misitu ya Kijiji cha Nanjirinji A zitafanywa kufuatana na mpango wa usimamizi wa Misitu uliokubalika na jamii ya Kijiji cha Nanjirinji A.

VIWANGO VYA ADHABU NA FAINI

8 i. Mtu yeyote atakayepatikana analima, kuchoma mkaa, kuweka makazi, kuchoma Misitu ovyo, kubangua asali, kuchimba madini au kukata kuni bila kibali atakuwa ametenda kosa chini ya sheria ndogo hizi na atalipa faini kwa kila kosa Shilingi elfu hamsini (50,000/=) na vifaa vyote vilivyotumika vitakuwa mali ya Kijiji na kulipia fidia ya uharibifu uliofanyika na gharama ya doria iliyofanyika au atashtakiwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha muda wa miezi sita(6) kwenda jela.

ii. Mtu yeyote atakayekutwa anavuna au atakayekamatwa na

magogo au mbao atalipa faini ya Shilingi elfu hamsini (50,000/=) na majengo au nguzo kwa ajili ya biashara bila ya kibali atalipa faini shilingi elfu hamsini (50,000/=) na vifaa na mali itakuwa mali ya Kijiji au atapelekwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha muda wa miezi sita (6) kwenda jela.

iii. Mtu yeyote akipatikana anaondoa au kubadili alama za mipaka ya Misitu zilizowekwa atakuwa ametenda kosa na atalipa faini shilingi elfu hamsini (50,000/=) na kurudishia alama zote kwa gharama zake au kupelekwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha muda wa miezi sita (6) kwenda jela.

iv. Mtu yeyote akipatikana na hatia ya kuchimba mawe, mchanga au udongo ndani ya Misitu atalipa faini shilingi elfu hamsini (50,000/=) na vifaa vilivyotumika kuwa mali ya Kijiji au atapelekwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha muda wa miezi sita (6) kwenda jela.

v. Mtu yeyote akipatikana na hatia ya kuingia Msituni bila utaratibu maalum kwa ajili ya kuchukua dawa za tiba, matunda, miyaa, ukindu, fito, kongowele, udongo, nyasi, miswaki, pikicho au mboga kwa ajili ya matumizi ya nyumbani tu atalipa faini kwa kila kosa shilingi elfu kumi (10,000/=) na kupewa onyo kali.Akirudia tena atafikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha muda wa miezi sita (6) kwenda jela.

vi. Kuchunga mifugo ndani ya Misitu faini kwa kila mnyama shilingi elfu ishirini (20,000/=).Kwa kipindi chote mifugo hiyo itakuwa chini ya mamlaka ya serikali ya kijiji na mmiliki wa mifugo hiyo atalazimika kulipia gharama za uharibifu utakaojitokeza kwenye misitu. Akikaidi atafikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha muda wa miezi sita (6) kwenda jela.Kuchunga mifugo ilyokamatwa kwa uhalifu kwa siku ni shilingi 20,000/=.Mifugo hiyo ikikaa kwa muda wa siku saba (7) bila ya mwenyewe kujitokeza itataifishwa na kuwa mali ya kijiji.

vii. Vyombo vya uchukuzi vitakavyokamatwa vikisaidia uchukuzi wa mazao ya misitu yaliyovunwa kiharamu/bila kibali vitatozwa faini zifuatazo;baiskeli 30,000/=,pikipiki 500,000/= na gari 1000,000/= na mazao ya misitu yaliyokamatwa yatataifishwa.Akikaidi atafikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha muda wa miezi sita (6) kwenda jela.Akipatikana na kosa atalipa gharama ya doria iliyofanyika/iliyomkamata.

viii. "Kiongozi" akipatikana na hatia ya kuhusika katika kukiuka mojawapo ya taratibu zilizowekwa na sheria hii faini yake ni shilingi elfu hamsini (50,000/=), kurudisha gharama pamoja na kulazimika kujiuzulu madaraka aliyonayo au atapelekwa Mahakamani.

ix. Kama kiongozi atathibitika kuona, kusikia au kufahamu uhalifu unafanyika na kuunyamazia kimya fani yake ni

shilingi elfu hamsini (50,000/=) na kuondolewa madarakani au atapelekwa mahakamani.

x. Kama mtu yeyote ataizuia Kamati ya Maliasili kufanya kazi zake kwa kutishia au kutoa maneno ya kashfa atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) au atafikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha muda wa miezi sita (6) kwenda jela.

xi. Mtu yeyote ambaye ataenda kinyume na sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kujaza fomu ya kukiri makosa kama zitakavyo andaliwa na Kijiji kabla ya kulipa faini.

xii. Mtu yeyote katika sheria ndogo hizi ambaye atakataa kulipa faini au kujaza fomu ya kukiri makosa atafikishwa mahakamani.

xiii. Vifaa vyote vitakavyokamatwa ukiondoa mashine ya mnyororo(chainsaw) kutokana na makosa yaliyotajwa katika vifungu (i-vii) vitataifishwa na kuuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Kijiji na fedha zitakazopatikana zitakuwa mali ya Kijiji.

xiv. Bila kuathiri kifungu kidogo cha 13 (xiii) endapo mbao na magogo vitakuwa vimekamatwa Kijiji kitatakiwa kipate ruhusa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ndani ya siku thelathini (30) kabla ya kuuza au kutumia vitu hivyo.

xv. Mtu yeyote akipatikana na hatia ya kuwinda wanyama au uvuvi wa samaki bila kibali Kijiji kitawasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya kwa hatua zaidi kama zilivyo katika sheria ya Wanyama pori na uvuvi

xvi. Endapo mhalifu yeyote atakuwa amekamatwa na mnyama/nyama pori, Kijiji kitatakiwa kuwasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya mara baada ya kumkamata mhalifu kwa hatua zaidi kama zilivyo katika sheria ya Wanyama pori.

xvii. Mtuhumiwa yeyote atakayefikishwa mahakamani na kutiwa hatiani atalipa asilimia mia moja (100%) ya gharama za kesi.

9. Matumizi ya kifungu chochote ya sheria ndogo hizi yakileta utata, sheria mama ya Misitu na wanyama pori itatumika baada ya kupata ufafanuzi, maelekezo ya kitaalam na ushauri wa kisheria kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mpango wa usimamizi wa Misitu na Sheria ndogo hizi zimekubaliwa na kupitishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Nanjirinji A uliofanyika tarehe 10/6/2018.

Jina la Mwenyekiti wa kijiji.....

Sahihi.....

Tarehe.....

Jina la Mtendaji wa Kijiji .....

Sahihi.....

Tarehe.....

Mpango wa usimamizi wa misitu na Sheria hizi zimepitishwa na Kamati Maendeleo la Kata ya ..... (WDC) uliofanyika tarehe .....

Sheria ndogo hizi zimepitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa uliofanyika tarehe ..... na zitaanza kutumika tarehe **xx/xx/2018**.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa

Jina.....

Sahihi .....

Tarehe.....

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa

Jina.....

Sahihi .....

Tarehe .....